Kublogu kwa Matumaini



Hii ni sanaa ya mtaani inayopatikana huko Burma kwa lengo la kueneza uelewa kuhusu VVU na UKIMWI. Utoaji taarifa nchini Burma unafuatiliwa na kudhibitiwa kwa karibu, unachujwa na kuwekewa vizingiti. Habari za VVU nchini Myanmar hutumia blogu ili kufanya zipatikane. him.civiblog.org

Utangulizi: "Kublogu kwa Matumaini" (Blogging Positively)

Mwongozo huu wa "Blogging Positively" ni wazo la wanablogu kutafuta njia mwafaka ya kukabiliana na VVU/UKIMWI. Zana za uandishi wa kiraia - ikiwa ni pamoja na blogu, podikasti, na tovuti za picha za video – zinatoa fursa mpya na zenye ufanisi kwa wanaharakati wanaolenga kueneza ufahamu na kukuza mjadala kuhusu VVU/UKIMWI na unyanyapaa wa kijamii. Kuna njia nyingi tu zinazoonyesha kwamba blogu ni zana muhimu sana ya majadiliano na uanaharakati dhidi ya VVU/UKIMWI, ikiwa ni pamoja na: 1) unachochapisha ni sehemu ya kumbukumbu ya kudumu, inayohifadhiwa; 2) hadhira yako, kimsingi, ni ulimwengu mzima; 3) mawasiliano ya kibinafsi huwa hufanyika katika ngazi tofauti, kuanzia mahalia hadi kimataifa, 4) kutokujulikana inawezekana, na si kikwazo cha ushawishi; 5) na kuiga na kuchangaya kunatoa fursa ya kutia ubunifu katika usimuliaji; na 6) mazungumzo yanaweza kuwa ya wakati huohuo (kwa watu walio katika ukanda mmoja wa wakati) au katika kanda tofauti za wakati. Pia kuna uwezekano wa kuwepo hatari katika kublogu, na ni muhimu kuzizingatia, zikiwemo 1) hatari ya kueneza habari potofu; 2) kuwepo na uwezekano wa maoni yasiyo mazuri, na 3) ukosefu kompyuta, mtandao wa intaneti, na kukosekana kwa umeme. Katika utafiti wetu juu ya kublogu kuhusu VVU / UKIMWI, tumegundua wanablogu wapatao 200 duniani kote, wengi wao wanaishi na VVU / UKIMWI, ambao huandika mara kwa mara mada zinazohusu VVU / UKIMWI. Kwenye ramani yetu inayoruhusu kuingiliana

Katika Mwongozo Huu:

Kwa nini kublogu kuhusu VVU/UKIMWI?	2
Kwa wanablogu wapya	3
Kwa walimu na wawezeshaji	4
Masuala ya kisheria	5
Visa mafunzo	6
Jinsi ya kuanza	7
Ushauri kutoka kwa mkongwe	8

Rising Voices ni taasisi ya uandishi wa kiraia iliyoanzishwa na Global Voices [www.globalvoicesonline.org]. Kwa kuwaunganisha wapenzi wa kublogu, kutuma podikasti, na kutayarisha video kutoka duniani kote, ni matumaini yetu kwamba kila jirani kutoka kila makazi anapata fursa ya kushiriki katika mazungumzo ya mtandaoni yanayoenea kila mahali ulimwenguni. Mwongozo huu – wa Blogging Positively – ni wa pili katika mfululizo wa machapisho yanayokusudiwa kufanya ulimwengu wa uhabarishaji shirikishi uwe mwepesi kuelewa na mtu kujishirikisha. Tafadhali tembelea pia Utangulizi tuliokuandalia kuhusu Uandishi wa Kiraia: http://rising.globalvoicesonline.org/guides

Ramani ya wanablogu wanaoblogu kuhusu VVU/UKIMWI duniani kote. Toleo jipya hupatikana kupitia http://globalvoicesonline.org/specialcoverage/world-aids-day-2008/

(kiungo kipo chini) kuna orodha ya wanablogu tuliowabaini, na tunakaribisha nyongeza kwenye mtandao wetu.

Mwongozo huu kwa upande fulani ni matokeo ya mfululizo wa mijadala isiyo rasmi iliyofanyika kati ya mwaka 2008 na 2009 na kundi la watu kutoka kila kada: wanablogu nguli na wale wachanga; watu kutoka mijini na vijijini; wale wanaotoka nchi zilizoendelea na zinazoendelea; baadhi yao wakiwa na uhakika wa kuwa na tarakilishi na huduma ya intaneti, huku wengi wakiwa na uhaba wa nyenzo hizo; watu ambao wanaishi na VVU na wale wasio na VVU; wale wanaoshughulika na VVU/UKIMWI, na watu wanaofanya kazi katika maeneo mengine, kama vile teknolojia, tiba ya madhira, sanaa, na elimu ya sekondari. Kile ambacho sisi wote tunacho ni hamu ya kujifunza zaidi kuhusu jinsi teknolojia inavyoweza kutumika kukuza afya na ustawi wa watu, na jinsi uandishi wa kiraia unavyoweza kushughulikia kwa ufanisi janga la VVU/UKIMWI. Kichwa cha habari cha mwongozo huu, kilibuniwa na Daudi Were ambaye ni raia wa Kenya, na kina maana nyingi: Ni matumaini yetu mwongozo huu utakuwa wenye manufaa kwa watu walioambukizwa na kuathiriwa na VVU/UKIMWI, na kwamba utawasaidia wale wanaolenga kueneza welewa kuhusu kinga, kuishi kwa misingi ya afya, na haki za binadamu.

Je, Kublogu Ni Nini?

Neno "blogu" ni ufupisho wa neno *weblog* na linaeleza aina ya tovuti ambayo huongezewa taarifa zaidi kwa mtiririko wa muda. Ni kama kama ilivyo baruapepe.

Tofauti ni kwamba badala ya kutuma barua pepe kwa mtu mmoja tu, unachapisha habari kwenye tovuti ambamo inaweza kusomwa na mtu yeyote duniani anayeweza kujiunga na mtandao wa Intaneti. Blogu nyingi huruhusu maoni, kuwawezesha wasomaji kuuliza maswali au kuongeza maoni yao kuhusu ulichochapisha. Hivi ndivyo jinsi mazungumzo yanavyoanza - mtu mmoja anaandika maoni yake na kisha wengine kuchangia mazungumzo. Baadhi ya weblogs maarufu hupokea zaidi ya maoni 100 kila mara taarifa mpya inapochapishwa, lakini idadi kubwa ya blogu huandikwa kwa ajili ya hadhira ya wasomaji wachache tu wenye malengo yanayofanana.

Kwanini Kublogu Kuhusu VVI/UKIMWI

Lengo kuu la kublogu mara nyingi ni kutoa simulizi binafsi. Hizi zinaweza kusaidia kuhabarisha na kuelimisha wasomaji, kuamsha uanaharakati, na kuibua mabadiliko. Wanablogu wanaweza kukusimulia simulizi za ndani ya nafsi, badala ya kutegemea mambo yaleyale ya kila siku au takwimu. Kublogu juu ya hali ya mtu ya VVU au changamoto za wanaoishi na VVU/UKIMWI inaweza kuwapa moyo, si mwanablogu tu bali hata wasomaji wake. Blogu inaweza kutoa fursa iliyo salama na mahali pasipo na ubaguzi. Kwa mfano mtu anayeomba tiba ya dawa za kupunguza makali ya VVU, anaweza kuwaelezea wengine mchakato. Au mtu huyo anaweza kuunda "Kitabu cha Kumbukumbu" cha kidijitali kwa ajili ya familia na wale anaowapenda ili kuhifadhi historia ya

Kublogu kwa Siri

Kuna sababu nyingi za kublogu huku ukitumia jina lako halisi, ikiwa ni pamoja na kutambulika, uaminifu, na sifa. Lakini baadhi ya watu wanaishi katika maeneo au katika hali ambapo kile wanachokiandika kinaweza kutishia usalama wao. Kwa sababu hii, Global Voices imeandaa mwongozo wa jinsi ya kublogu kwa siri na kuficha utambulisho wako mtandaoni.

advocacy.globalvoicesonline.org

Kulinda Haki za Binadamu

Kiunganishi cha WITNESS Video Hub ni tovuti shirikishi ambamo mtu yeyote, popote anaweza kuchapisha habari kuhusiana na haki za binadamu ambayo inaweza kutumika kuleta mabadiliko. Ikiwa umeshuhudia ukatili wa polisi, au aina yoyote ya ukiukwaji wa haki za binadamu, na ukapiga picha hiyo kwa kutumia simu yako ya mkononi au kamera, basi jifunze njia hii ya kuituma kwa usalama na kwa siri ili kuweka kumbukumbu ya kile kilichotokea na saidia kuzuia vitendo vya aina hiyo. hub.witness.org

familia na kuimarisha uhusiano wa wale wanaobaki. Wengi wa wale wanaoblogu juu ya VVU/UKIMWI wanalenga kutoa elimu na njia za kujikinga. Baadhi wanalenga upande wa imani zaidi, wakati wengine hujadili bila uoga kuhusu ngono, dalili za VVU/UKIMWI, na unyanyapaa. Utetezi wa kisiasa ni muhimu kwa wanablogu hasa wanapotetea ili huduma za tiba, programu za msaada, na uimarishaji wa uwezo kiafya ili viwafikie wengi zaidi.

Kwa Wanablogu Wapya

Kama wewe unablogu kwa mara ya kwanza, fikiria hakuanza na mada rahisi, unayoielewa vema na si lazima iwe kuhusu VVU/UKIMWI. Baada ya kuzoea kublogu basi itakuwia rahisi kushughulikia masuala yanayohusu na janga la UKIMWI. Wanablogu wengi wapya watajihisi wepesi zaidi kuanza taratibu, hatua kwa hatua, lakini wapo wanaoweza kuingia moja kwa moja. Inasaidia kufikiria kuhusu hadhira yako unapoandika. Unaweza kuanza kwa kuwaza kuhusu hadhira uliyoizoea, kisha kupanua wigo wako unavyozidi kujiamini. Kumbuka kwamba chochote unachochapisha kwenye blogu yako kinaweza kuonekana na mamilioni ya watu. Kutokana na uzoefu, blogu nyingi huwa na wastani wa wasomaji dazeni moja, lakini ni muhimu kutilia maanani umma unaoweza kuwasiliana nao kupitia blogu pale unapofanya uchaguzi kuhusu nini uchapishe. Daima ni vema kuomba ridhaa ya rafiki yako kabla hujachapisha habari au kumbukumbu inayomhusu. Kama ungependa watoto kusoma blogu yako ni muhimu kufikiria nini kisicho sahihi kwao kusoma. Vilevile unaweza pia kufikiri kuhusu njia ya kueneza ujumbe wako kwa wale ambao hawawezi kusoma. Mawasiliano kwa kuonyesha – ikiwa ni pamoja na video na picha - yanaweza kusaidia kufikisha ujumbe wako kwa watu wengi zaidi. Kwa wenye matatizo ya kuona, muziki na rekodi vinaweza kutumika kuwasilisha ujumbe wako. Makala ya blogu si lazima iwe ndefu, ya kitaalamu, au iliyotayarishwa vizuri sana. Kutokuwa rasmi ndiyo asili ya kublogu. Kilicho muhimu ni kwamba unafurahia mchakato na kujisikia vizuri kuhusu kile ambacho umefanya.

Kundi la Msaada la Ntwakgolo katika Kijiji cha Nata

Karibu kila mtu mmoja katika watu wazima wanne nchini Botswana anaishi na VVU, na Umoja wa Mataifa umekadiria kuwa kufikia mwaka 2010 zaidi ya asilimia 20 ya watoto wote nchini Botswana watakuwa yatima kutokana na janga la VVU/UKIMWI. Katika kijiji kidogo cha Nata wanaharakati 20 wanaishi kwa uwazi na hali yao ya VVU ili kukabiliana na unyanyapaa unaoendana na janga hili. Katika lugha ya KiSetswana (lugha rasmi nchini Botswana), "Ntwakgolo" ina maana ya "Vita Kuu," jina mwafaka kwa ajili ya vita inayopigwa dhidi ya VVU/UKIMWI kule Nata. Wanachama wa Kundi la Msaada la Ntwakgolo ni miongoni mwa watu wa kwanza kuweka wazi hali yao ya kuwa na VVU katika jamii zao. Kwa mfano wao, wanawahamasisha wengine kujitokeza hadharani pia. Weblog ya Kijiji cha Nata ilianza mwaka 2006 baada ya msafiri wa tech-savvy alipokutana na mwanaharakati mwelimishaji kuhusu VVU/UKIMWI katika kijiji hicho cha nchini Botswana. Blogu hii ilisaidia kukusanywa kwa makumi elfu ya dola na sasa inaendeshwa na wafanyakazi wa kijijini hapo wa Mfuko wa UKIMWI na Yatima wa Nata. http://is.gd/1B229 | http://is.gd/1B1Og

REPACTED

REPACTED ilianzishwa mwaka wa 2001 ili kuhamasisha vijana kujihusisha na maendeleo ya jamii kupitia maonyesho shirikishi, kampeni za uhamasishaji, elimu rika na ushauri nasaha. REPACTED inashughulikia VVU/UKIMWI, tatizo la dawa za kulevya, amani na utatuzi wa migogoro, na maendeleo endelevu. Mwaka 2008 walianzisha Youth Media Consultative Forum, ambayo hukusanya habari na taarifa kutoka katika jamii ndani na nje ya Nakuru, Kenya, na kisha kuzituma kwenye mtandao, ili kuwafanya wakazi wa maeneo hayo kuonyesha picha halisi kuhusu jamii yao. REPACTED imewapa mafunzo zaidi ya wafanyakazi 20 na viongozi wa kijamii juu ya jinsi ya kublogu na kuzalisha makala zinazoweza kutumika kwenye vyombo mbalimbali vya upashanaji habari. Wale ambao tayari wamepata mafunzo wanahimizwa kutafuta walau marafiki 20, ikiwa ni pamoja na vijana ambao wanajihusisha na vikundi visivyofaa.
http://www.repactedkenya.com

Kwa Wawezeshaji na Walimu:

Endapo unawasaidia wengine kuchapisha maudhui kwenye blogu, wahimize kuchangia mada kutoka moyoni na yanaoweza kuibuwa mjadala. Hii inapaswa kusaidia wageni kuwa na utulivu. Ingawa hatua za ju zaidi za kublogu zinaweza kuwa na ugumu wa kiufundi, ni vema kuweka mambo rahisi, yanayoeleweka, na yanayowafurahisha wanablogu wapya. Ni muhimu kuhimiza ushirikiano. Wakumbushe wanablogu wapya kuchangia maoni kwenye makala zilizochapishwa na wenzao. Wakati mwingine pia inasaidia kuweka sehemu ya "makala ya mgeni" kwenye blogu ya mtu mwingine. Wanablogu wengi tofauti pia wanaweza kuchangia blogu ya kikundi, hiyo inahamasisha hali ya kazi ya pamoja. Kama una muda, anzisha blogu yako mwenyewe, na weka viungo vya blogu za wanafunzi wako kwenye blogu yako. Kama unaweza kuwapata walimu au wawezeshaji wenzako ambao wana elimu stadi katika utunzi au kuandika hadithi, unaweza kuomba masaada wao. Huenda watajuwa mbinu za kuwezesha watu kuwa na utulivu na kufurahia mchakato wa ubunifu. Wanaweza kuwa na muda zaidi kuliko wafanyakazi wa afya au mashirika ya huduma ambao mara nyingi huwa na kazi nyingi sana. Shule na maktaba zinaweza pia kuwa na rasilimali watu wenye ujuzi unaoweza kusaidia. Fikiria jinsi ya kutoa nafasi zaidi kwa wale wasio na uelewa wa Intaneti. Nchini Uganda, mradi wa PeerLink [http://www.geocities.com/ peliug / index.htm] huunganisha kujifunza juu ya kompyuta na kujifunza kuhusu VVU/UKIMWI. Wanafunzi wa mijini, ambao huwa na ustadi wa kutumia kompyuta, huunganishwa na vijana katika shule za vijijini, ambao mara nyingi wanakosa vifaa na maarifa kuhusu kompyuta, pamoja na kupata Intaneti. Vijana wa mijini huwapa msaada wenzao wa vijijini kupata huduma ya vifaa vya kompyuta na Intaneti, na kisha kutoa miongozo ya kompyuta kwa wanafunzi wa vijijini. Makundi haya kisha hushiriki katika kujifunza pamoja juu ya VVU/UKIMWI.

Maswali na Majibu kwa Walimu au Wawezeshaji Jinsi gani tunaweza kuhamasisha vijana, wanawake, walemavu, wanaoishi na VVU/UKIMWI, na wengine ambao mara nyingi ni wanyonge?

Watu wakikuijia, waandalie mazingira yaliyo salama ili waanze kuonja hali ya kuwa wanablogu. Vinginevyo, unaweza kuzitembelea taasisi zinazojishughulisha na watu hawa, ili kuhamasisha wazo la kublogu kama zana inayokuza uwezo na vilevile kama zana ya kutolea elimu.

Je, jinsi gani tutumie zana za upashanaji habari ili kuunda harakati za kijamii kuleta mabadiliko?

VVU/UKIMWI ni changamoto ya kiafya kwa kila mtu na kwa jamii vilevile. Kwa sababu ya taathira yake iliyoenea katika nyanja tofauti za maisha na katika ngazi tofauti za kijamii, ni jambo ambalo kwalo vuguvugu la kijamii linaweza kuundwa kwa urahisi. Wanablogu wanaweza kuhamasika kuona kazi zao zikiunganishwa na mitandao mipana zaidi, maana zana mpya za habari huunganisha vikundi vya mahali, kitaifa na duniani kote. Wanablogu wanaoishi na UKIMWI wanaweza kuanzisha mawasiliano na wengine wenye hali kama zao na hata wengine wanaokabiliana na mataizo mengine. Kublogu inaweza kuwa njia yenye ufanisi katika kuwafikia wale wasio au walio na welewa mdogo kuhusu VVU/UKIMWI – au hata wale wenye mitazamo tofauti kuhusiana na janga hili – kujenga uhusiano na kuchagiza majadiliano.

Jinsi gani tunaweza kuhusisha taasisi na wataalamu wa afya?

Kublogu kunaweza kutangazwa kama aina ya tiba kwa wateja na wafanyakazi wao, na taasisi zinaweza kuhamasishwa kublogu kuhusu mafanikio, mahitaji, na changamoto zao. Baadhi ya taasisi na wataalamu wa afya wanaweza kuwa na uwezo wa kufundisha wanablogu wapya, na wanaweza kutoa vifaa vya kuelimisha wanablogu kufikisha taarifa za VVU/UKIMWI kwa wengine. Taasisi zinaweza kusaidia upatikanaji wa huduma ya Intaneti, wanablogu kwa upande mwengine wanaweza kuunda vikundi vya waelimishaji rika, kufanya

Vitabu vya Kumbukumbu vya Kidijitali

Waganda wanaopata mafunzo kwa ajili ya mradi wa "Kitabu cha Kumbukumbu" ambao hufundisha wazazi walio na VVU kuwasiliana na watoto wao kuhusu masuala magumu ya VVU, kifo, na mipango ya mali wanayoiacha. Mradi wa "Kitabu cha Kumbukumbu" ulianza na wahamiaji wa Kiafrika waliogua mahututi sana nchini Uingereza ambao hawakutaka watoto wao wasahau kuhusu urithi wa utamaduni wao. Kijadi vitabu vya kumbukumbu hutengenezwa kwa karatasi, picha, na wakati mwingine vipande vilivyokatwa kwenye magazeti. Kutengeneza kitabu cha kumbukumbu cha kidijitali kunaruhusu familia na marafiki nao pia kuingiza video, nyimbo wanazozipenda sana, nasaba za kifamilia, picha za kidijitali, na hata maandishi.

Mpango wa mafunzo umeeneza mradi wa kitabu cha kumbukumbu kote nchini Uganda, na ushirikiano umesaidia kupanua matumizi yake katika nchi nyingine za Kiafrika, ikiwa ni pamoja na Kenya, Zambia, Zimbabwe, Ethiopia, Tanzania na Afrika Kusini. Baada ya kutayarisha kitabu cha kumbukumbu mshiriki mmoja alieleza: "Sina wasiwasi juu ya mustakabali. Kitabu cha Kumbukumbu na mafunzo vimenisaidia kuwaelezea watoto wangu kwamba mimi niko na VVU na kwamba siku moja nitafariki, kwa hiyo nimeweza kuwaandaa. Lakini nimeeleza pia kwamba kila mmoja kuna siku atakufa, na ndiyo itakavyotokea kwangu."

AZUR Development na AIDS Rights Congo

Katika Jamhuri ya Kongo, AZUR Development hutoa mafunzo kwa maafisa wa mawasiliano wa mashirika yanayojishughulisha na VVU/UKIMWI kwa usimuliaji hadithi kwa njia za kidijitali, redio za mtandaoni, na kublogu ili kuweka kumbukumbu ya ubaguzi wanaoteseka nao watu walioambukizwa na kuathiriwa na VVU/AIDS. Simulizi hizi hutumika kama nyenzo za kuendeshea utetezi, elimu, na kukuza haki za watu wanaoishi na VVU. Kila afisa wa mawasiliano huelezea jinsi ambavyo VVU/UKIMWI huathiri jamii kwa sasa pale anapofanyia kazi, na jinsi maisha ya kila siku yalivyo kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI. Mradi huo unaitwa AIDS Rights Congo. Katika mwaka wa 2006, AZUR Development ilifanya mradi ili kuona jinsi ya kutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa watu 100 waliokuwa wakiishi na VVU/UKIMWI. Wengi wa watu hawa walikuwa wanawake wanaoishi katika Pointe-Noire, Congo. Kupitia huu mradi, waligundua ni kwa kiwango gani wanawake hawa walikuwa wamenyang'anywa mali zao, na kutelekezwa na wenzi na familia zao. Mradi ulianzisha kazi ya Azur Development ili kutetea haki za watu wanaoishi na VVU. Wao pia wanaratibu Mtandao wa UKIMWI Afrika, ambapo wanatumia blogu ili kusimulia visa, ushuhuda, na shughuli kuhusu VVU/UKIMWI na malaria kutoka miongoni mwa wanachama wa mtandao huo. Wametayarisha warsha mbalimbali kuhusu matumizi ya kompyuta na Intaneti. http://www.azurdev.org/en, azurweb.blogspot.com aidsrightscongo.org

Kwa Mashu Community Advancement Projects

Mwaka wa 1998, Gugu Dlamini mwenye miaka 36 alipigwa mawe hadi kufa na umati wa watu kule Kwa Mashu, mji wa Durban, Afrika Kusini. Kabla ya kifo chake, alikuwa ameweka wazi hali yake ya VVU katika mkutano wa kuhamasisha uelewa wa UKIMWI. Wengi wanaamini kifo chake ni matokeo ya moja kwa moja ya kuvunja kwake ukimya kuhusu hali yake ya kiafya. Kwa matumaini ya kuzuia matukio ya kuhuzunisha namna hiyo, Kwa Mashu Community Advancement Projects (K-CAP) imewapa mafunzo vijana 20 kutoka mji huo kuwa waandishi habari wa kiraia wakitoa taarifa juu ya masuala ya afya, hasa kuhusiana na VVU/UKIMWI. Takribani watu milioni 5.7 nchini Afrika ya Kusini wanaishi na VVU/UKIMWI, na watu 350,000 walikufa kutokana na ugonjwa huo katika mwaka wa 2007. K-CAP inapatikana katika sehemu ya Kwa Mashu Township ambapo maambukizi ya VVU yako juu zaidi. http://www.kcap.co.za | http://is.gd/1B7gM

kazi sambamba na taasisi ili kukuza ubora wa afya ya jamii.

Jinsi gani tunaweza kukuza na kuendeleza kublogu ili kuwahimiza watu kujiona kama viongozi?

Kama kila mtu anaelewa kuwa sauti yake kupitia blogu ni ya kipekee na inaweza kuwatia moyo wengine kuelewa vema zaidi suala zima la au kuwa motomoto katika kushughulikia VVU/UKIMWI bila shaka hii itawachochea kuzungumza waziwazi.

Kublogu ni njia ya kuwezesha kwa sababu kila mmoja anaweza kuitumia, kama mazingira yakiandaliwa basi inaweza kuwa muhimu katika kujenga kujiamini zaidi na kujipatia maarifa mbalimbali. Uongozi hutokana na kajihisi kuwa mmiliki.

Jinsi gani tunaweza kushughulikia hofu ya kutojulikana kuhusiana na Kublogu kwa mara ya kwanza?

Kuanza kublogu kwa kushugulia mada nyepesi kiasi na kisha kupanda ngazi ili kushughulikia VVU/UKIMWI inaweza kuwa njia ya kushughulikia hofu kuhusu yasiyojulikana. Hata hivyo, wakati mwingine watu hujihisi kuwa na haraka ya kushughulikia mada hiyo, hasa kama ina athiri maisha yao. Mazoezi ya mara kwa mara ya kublogu, pamoja na mazingira mwafaka na shughuli za kujenga uwezo, yote haya hayana budi kupunguza hofu na badala yake kuongeza kujiamini, au walau uwazi katika kujifunza kuendeleza stadi mpya.

Jinsi gani tunaweza kuwawezesha watu kublogu wenyewe, na pia kuwafundisha wengine?

Uwiano katika kujieleza na kuwepo kwa elimu rika ni muhimu. Waombe watu watenge muda wa kublogu mara kwa mara, na wasaidie kupata mianya ya kutangaza kazi zao. Wahamasishe watu kujiona kama viongozi, na wasaidie kuelewa jinsi elimu rika ilivyo ya thamani na muhimu, kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya VVU/UKIMWI na kwa ujumla wa ustawi wao wenyewe, familia zao na jamii. Kuelekeza juhudi zao katika muktadha huu mpana zaidi bila shaka utawatia moyo watu kutaka kushirikishana, kufundishana, na kuongeza juhudi katika VVU/UKIMWI, na changamoto kwa ajili ya maendeleo endelevu ya watu.

Nukuu na nakili kutoka kwa Wanablogu Wanaoishi na VVU

Just for kiks

"Mimi nilianza kusoma zaidi kuhusu virusi na watu ambao wemeambukizwa. Mimi ni mmoja wao sasa na ni lazima nijifunze namna ya kukabiliana hali hiyo. Kupambana na adui asiyejulikana kwa hakika ni vita iliyopotezwa tangu mwanzoni. Mimi niliongea na marafiki wa marafiki na kisha tukaanzisha kikundi. Tuliongelea masuala mbalimbali na hali na uzoefu: lishe, vitamini, mchangayiko wa dawa na vidonge wanavyomeza kila siku na ambavyo ninahofia kuanza kuvitumia mapema, afya njema katika maisha ya ngono, ngono na uwajibikaji, dawa za kulevya, na kwa nini tusizitumiea kamwe, kuwafikia vijana, kuwafikia watu ambao hawajaambukizwa, kuwafikia watu wasiojua chochote kuhusu kuambukizwa. Na ndiyo, kuwafikia watu ambao hawataki kuelewa tatizo hili. " Mahali: Hong Kong http://bikolanongtsekwangbakla.blogspot.com/

Shajara ya Justin ya VVU

Kama ambavyo wengi wenu mnafahamu, mimi ni mzungumzaji sana kuhusu mimi ni nani na kuhusu uelewa wa VVU, Kinga na Elimu. Nilipobaini kuhusu hali yangu sikujua nini cha kufanya, lakini nilijua kwamba lazima nifanye kitu fulani ili nipate msaada na kuwasaidia wengine. Kwa hiyo nilibuni *Shajara ya Justin ya VVU*. Familia yangu waliniunga mkono lakini jambo hili lilielezwa kwa wale tu waliokuwa na umri wa kutosha kuelewa kuhusu ugonjwa huo. Nina wadogo zangu wawili wadogo ambao ninawapenda sana, majina yao ni Josh na Brandon. Wao ni wadogo kwangu, kwa hiyo nilijihisi ninawajibu wa kuwalinda au walau picha waliyo nayo juu yangu. Mara tu unapoweka wazi kuhusu hali yako ya VVU ni karibu wazi kwa kila mtu, hasa kama wewe ni mwanaharakati mkubwa wa VVU kama mimi, ambaye hajali kuhusu kuwashirikisha wengine habari zake binafsi. Josh na Brandon, najua mligundua kuhusu hali yangu ya kuishi na VVU kupitia Intaneti, nilitaka tu kuwaambia kuwa ninawapenda sana na kila kitu kiko sawa, mimi ni mzima." Mahali: Marekani http://justinshivjournal.blogspot.com

有了愛滋~還能擁有愛嗎?

Maelezo: Kwa miaka 3, Guan De amechapisha na kushirikisha kuhusu maisha yake kama mtu anayeishi na VVU kupitia blogu yake. Ni mtu jasiri na mwenye matumaini kuhusu hali yake. Bado ana shauku ya kutaka kupenda na kupendwa. Mahali: Taiwan http://mypaper.pchome.com.tw/news/lmo861/ http://mypaper.pchome.com.tw/news/lmo861/

Tawasifu ya mtu aliye na VVU

"Nilipokuwa nikikaa Kathmandu, nilisikia kuhusu shirika lisilo la kiserikali ambalo hutoa huduma na mafunzo kuhusu VVU/UKIMWI. Nilijiunga nao na kuanza kupata mafunzo mengi. Limenionyesha upande ulio chanya wa maisha. Waliniambia kuwa VVU/UKIMWI huwezi kutibiwa kikamilifu, lakini kuna dawa ambazo zinaweza kusaidia kupunguza kasi ya kudidimia kwa mifumo yetu ya kinga mwilini na kutusaidia kuishi kwa muda mrefu tukiwa wenye afya njema. Dawa hizi hugawanywa bure katika hospitali za serikali. Tunaweza kuishi miaka mingi kama waishivyo wengine wasio na maambukizo. Ni jambo linalonipa faraja sana. Mume wangu na mimi tulianza matibabu ya dawa za kurefusha maisha huko. Mafundisho na mipango yao hunitia hamasa kubwa. Inavunjilia mbali miiko na simulizi nyingi kuhusu VVU/UKIMWI ambazo nimewahi kusikia. Hilo limenipa furaha zaidi maishani mwangu, ambayo nilikuwa nimepoteza miaka mingi iliyopita. Kisha nikaanza kufikiria, ni kwa nini aina hii ya mipangilo hazipatikani katika kijiji chetu, Achham, nami nilijitia moyo kuanzisha moja katika kijiji yangu." (Imeharirwa ili ieleweke) Mahali: Nepal http://autobiography-of-an-hiv-positive.blogspot.com/

Back in the Closet

"Mnamo mwezi Juni mwaka 2008, kama ninakumbuka vizuri, nilipata taarifa ya idadi ya CD4 zangu kwa mara ya kwanza wakati nilipokuwa bado katika Hospitali ya San Lazaro. Na ilikuwa 343. Na ilipofika mwezi Agosti, nilihamishiwa RITM, ambapo walichukua upya vipimo vya taarifa ya msingi ya ugonjwa wangu. CD4 zangu zilikuwa zimeshuka hadi 328. Ndani ya miezi 2 tu zilikuwa zimeporomoka pointi 15. Nafikiri ilikuwa kwa sababu ya mtanziko wa mawazo na wasiwasi uliosababishwa na kikomo hicho nilichoelezwa pale San Lazaro; kwamba ilinipasa kumpata mtu katika familia yangu wa kumweleza tatizo langu kabla sijaanzishiwa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Sikuwa tayari kwa jambo hilo." Mahali: Ufilipino.

http://backinthecloset.blogspot.com/

Masuala ya kisheria

Kwa wanablogu, ni vizuri kutochapisha mtandaoni kile ambacho katika hali ya kawaida usingekisema. Japokuwa ni jambo linalotokea kwa nadra sana, wanablogu wanaweza kushitakiwa kwa kashfa na kutoa madai ya uongo kama watakuwa wametoa taarifa zisizo za kweli za mtu au kikundi fulani na taarifa hizo ziwe zinawavunjia heshima mbele ya jamii. Ni muhimu kwamba kamwe usieleze mtandaoni hali ya mtu mwenye VVU labda kama umepata ridhaa yao kufanya hivyo. Kuna pendekezo la "Kanuni ya Maadili" kwa wanablogu na kublogu, inapatikana katika http://www.is.gd/1CaWG. Blogger.com imechapisha miongozo kwa ajili ya blogu na wanablogu [blogger.com/content's] ambayo inaleta uwiano katika uhuru wa kujieleza na wajibu na heshima kwa watu wengine. Miongoni mwa maudhui wasiyoruhusu ni picha za ngono; hotuba za kuchochea chuki na vurugu; ukiukwaji wa dhahiri wa haki miliki; taarifa binafsi na za siri; maudhui yanayochagiza shughuli za hatari za zilizo haramu; na makala kutoka kwa mtu yeyote kujaribu kujifanya mtu mwingine. Kwa rejea kwa ajili ya makala zaidi za kisheria kwa wanablogu zinapatikana katika citmedialaw.org/legalguide

Kuanza: Vidokezo muhimu kwa wanablogu wapya

Kuna mamia ya machapisho ya kujifunzia na miongozo inayoeleza mambo ya misingi ya kublogu na masuala yote ya vyombo vya habari vya kidijitali. Kila unapokuwa na swali unaweza kutembelea http://google.com, andika swali lako kisha bofya kifungo cha tafutizi. Unaweza pata jibu linalokaribia swali lako. Katika sehemu hii tutajiunga na miongozo michache ambayo bila shaka itakusaidia kuanza kublogu.

Kuchagua programu ya kublogu.

Hatua ya kwanza ni kuchagua huduma itakayohifadhi blogu yako. Zipo huduma za kublogu mbili zilizo maarufu (na za bure!) ni: http://wordpress.com . na http://blogger.com. Blogger inamilikiwa na Google na inaingiliana vema na bidhaa nyingine za Google. WordPress imejikita kwenye programu iliyo wazi na inawapa watumiaji wake fursa ya kuifanya ya kwao zaidi. Huduma zote mbili ni nzuri sana, na unaweza daima kubadili kutoka moja hadi nyingine. Wanablogu wa Afrika wanaweza pia kutumia http://maneno.org , ambayo inawalenga wanablogu wa Afrika katika maeneo yenye kasi ndogo ya uunganishaji wa Intaneti. Pia imezingatia utumiaji wa lugha nyingi pamoja na tafsiri.

Maelezo ya kujifunzia na Miongozo ya WordPress:
- http://en.flossmanuals.net/wordpress
- http://support.wordpress.com/
- http://lorelle.wordpress.com/wordpress-resources

Maelezo ya kujifunzia na Miongozo ya Blogger:
- http://www.blogger.com/tour_start.g
- http://bloggerfordummies.blogspot.com/
- http://is.gd/2oFem

Vidokezo na Mapendekezo kwa Wanablogu Wapya:
- http://www.blogtips.org/start-blogging-but-what-will-you-blog-about/
- http://www.toptenblogtips.com/
- http://is.gd/2oFw4

Ukisoma baadhi ya kurasa za mitandao ambayo viungo vyake tumeweka hapo juu, basi utakuwa na taarifa za kutosha kukusaidia kuanza. Hatimaye unaweza pia kuanza kupachika picha, sauti za kunaswa, na video kwenye blogu yako. Pia tazama mwongozo wa "Introduction to Citizen Media" ili kupata picha ya jumla kuhusu uandishi wa kidijitali mtandaoni.
[Http://rising.globalvoicesonline.org/projects/guides]

Mwongozo wa Radio, Video za Mtandaoni, na Picha:
- http://www.podcastfreeamerica.com/
- http://www.kcnn.org/mitv/
- http://tlc.ousd.k12.ca.us/ ~acody/digi1.html

Taarifa za VVU nchini Myanmar

Jamie Uhrig, mwanaharakati wa afya, mwanablogu, na msimamizi wa Taarifa za VVU nchini Myanmar (http://him.civiblog.org/) ambayo inatoa baadhi ya vidokezo kwa ajili ya "kublogu na zaidi ya hapo," hasa katika maeneo ambayo yana kasi ndogo ya Intaneti au haipo kabisa.

"Blogu ni nyenzo bora sana ambazo zinaweza kutumikia watu wengi," anasema Uhrig, lakini anaonya kwamba kuna wakati mwingine "ni vigumu kupata huduma kwa kwa wanajamii katika maeneo mengi yanayoendelea duniani," hasa pale zinapohusishwa picha za video na usanifu mzito. Uhrig pia anabainisha kwamba baadhi ya serikali kandamizi huzuia kupeperushwa au kusomwa kwa maudhui wasiyoyapenda, na kwamba ni muhimu katika hali kama hizo kufikiria njia mbadala ya usambazaji kama vile baruapepe. (Kwa mengi zaidi kuhusu kublogu bila kujulikana na kukwepa kunyamazishwa, tafadhali tazama mwongozo wa "Blogging Anonymously" ulioambatanishwa kwenye ukurasa wa 1.)

Chapisho la kwenye blogu linaweza kunakiliwa kwenye barua pepe na kusambzwa kwa wapokeaji kadhaa. Uhrig anasisitiza kuwa Gmail ya Google inaweza kuwa salama kiasi kwamba serikali na macho mengine yanayopeleleza hawawezi kuona ujumbe wako: http://him.civiblog.org/blog/_archives/2008/12/2/4003413.html Uhrig pia anahimiza wanaharakati wenzake kutumia simu za mkononi. Skype [www.skype.com] inaweza kutumika kwa urahisi kutuma ujumbe mfupi wenye maandishi mengi kwa simu za mkononi duniani kote na kwa bei nafuu. FrontlineSMS [http://www.frontlinesms.com] ni mfumo wa kutuma na kupokea ujumbe mfupi ambao unaruhusu mashirika yasiyo ya kiserikali kuwasiliana na dazei au hata mamia ya wenzao papo hapo. Vinavyohitajika ili kufanikisha ni simu ya mkononi na kompyuta.



Ushauri Kutoka kwa Mwanablogu Mkongwe

Brian Finch Mwanablogu kutoka Canada anayeishi na VVU, mwanaharakati wa kijamii, mcheshi, na mwanzilishi wa "Acid Reflux," inayojulikana kama " HIV's First Blog Reality Show " http://acidrefluxweb.com

"Intaneti huwezesha uwanaharakati wa kiteknolojia. Humpa mtu binafsi sauti na udhibiti, kujieleza kwa njia anayoona inafaa. Ni kumiliki nguvu tena, na kuunda sauti ambayo mwingine hawezi kuichukua. Kwangu binafsi, ni njia ya kujieleza mwenyewe nje ya sanduku dogo la VVU, na kuwepo nje ya ruwaza ya ugonjwa huo.

"Kadiri watu wengi zaidi wanavyozidi kuandika waziwazi kuhusu hali zao, ndivyo kadiri hiyo. Uwepo 'wa wazi' wa mtandaoni unatoa chagizo kubwa kwa wengine. "Hakuna historia inayoonyesha kwamba VVU/UKIMWI ni ya jamii ya watu fulani tu, ukiachia mbali historia kwamba ni tatizo la kimataifa. Nchi nyingi wana ubinafsi. Intaneti imesaidia kuvunjilia mbali hali hiyo. Kwa mfano, tovuti inaweza kuonekana na watu wengi duniani kote. Hasa kwa wanawake, walioko Afrika na kwingineko, intanet imekuwa ni mtandao wa kuafikiana na kutiana moyo wa faraja.

"Malengo ni ya kibinafsi sana. Mtu anapokuwa wazi juu ya hali yake, malengo yanaweza kuwa mengi ya kindani kama vile ya kiinje. Lengo moja linaweza kuwa juu ya kuboresha uchapishaji habari za VVU/UKIMWI, na kuhamasisha welewa wa jumla. Lingine linaweza kuwa tendo la uwezeshaji, kuwatia wengine changamoto au hata jamii yako – vyovyote vile unavyotaka iwe – kuhusiana na nini inaweza kuwa maana ya kuwa mtu unayeishi na VVU.

Ndio sababu mimi hutumia ucheshi katika kazi yangu mwenyewe na kuweka mipaka. "Nimeona kwamba watu wengi hupenda kuandika kuhusu jinsi walivyojikuta pale waliopo na wakati huo. Ni vigumu kuweka njia bora, lakini ningelipendekeza kuanza kuandika yale unayoweza kusema katika mazungumzo yoyote. Utangulizi na historia huja kwanza. Kisha jibu maswali zaidi: Kwa nini unaandika? Unatarajia kupata nini kutokana na uandishi wako? Historia yako ikoje? Je, ni mambo gani unataka tufahamu kuhusu wewe, ili kukuona katika ukamilifu wako, kujiona tunahusiana na wewe? Kwa nini tutake kurejea kujua mengi zaidi? "Ucheshi ni njia ya Kurejesha nguvu... nimeshudia wale wasio na VVU wakijaribu kutuelezea na kututungia majina kibao. Kuna jambo moja ambalo hatupaswi kuwa, na hilo ni dhahiri ... kufurahia maisha, wakati ambapo wakati wote mtu huna budi kuwa mwanaharakati kwa kujitokeza waziwazi hadharani. Daima ucheshi umenivusha maishani, hasa katika nyakati nyingine zilizo ngumu sana. Nilipofahamu kwamba nina VVU, zaidi ya miaka ishirini iliyopita, sikujua kama nilie au nicheke. Nilichagua kucheka sana kadiri nilivyoweza. Ucheshi wenye kiza ulikuwa rafiki yangu nambari moja. Ninaupenda kwa sababu unashtua, wakati huohuo ukinipa ujasiri wa kukabili magumu. Ucheshi ulikuwa na umeendelea kuwa silaha yenye nguvu kukabili hali halisi zilizo chungu za maisha yetu. Unauchukua ubaya na kuubadili kuwa kitendawili kilichotiliwa chumvi mno, kwa hakika huishia kuwa jambo la kufurahisha. "

"(Kwa mfano wa matumizi ya ucheshi wa Finch, tazama Positively HIV-larious, http://acidrefluxweb.com/cat? = 184, Edition # 364, Januari 21 - Februari 4, 2009)

Zaidi ya Kublogu: zana zinginezo muhimu

Wakati mwongozo huu unalenga kublogu kushughulikia VVU/UKIMWI, kuna zana zingine mtandaoni zinazoshugulikia kampeni ya utetezi, kueneza ufahamu, na kujenga mtandao wa wanarika. Mitandao ya kujenga urafiki kama Facebook [http://www.facebook.com], MySpace [http://www.myspace.com], na Kabissa [http://www.kabissa.org] huruhusu watu binafsi na mashirika kutayarisha wasifu na kutafuta marafiki zaidi katika ngazi ya mtaa, kitaifa, na kimataifa walio na maslahi yanayofanana. DigiActive [www.digiactive.org] imechapisha miongozo kuhusu kutumia zana za mitandao ya kijamii kwa ajili ya kampeni za utetezi. Tactical Technology Collective [www.tacticaltech.org] ina miongozo mizuri ya kuelezea jinsi ya kutumia programu iliyo wazi kwa ajili ya wanaharakati. Mobile Active [http://mobileactive.org] inalenga katika kutumia simu ya mkononi kuleta mabadiliko ya kijamii na kuboresha huduma ya afya. Injini tafutizi za Blogu kama Technorati [http://technorati.com] inaweza kusaidia kutangaza blogu yako na kusaidia katika kutafuta blogu nyingine zinazoweza kukuvutia.

Kujiunga na Mazungumzo ya Ulimwengu

Sasa kwa kuwa unaelewa misingi ya kublogu, ni wakati wa kujiunga kwenye mazungumzo ya kiulimwengu. Global Voices ni jamii watu wenye shauku ya uandishi wa kiraia kutoka pande zote duniani ambayo hukusanya, huchanganua, na kupaaza mazungumzo yanayoendelea mtandaoni. Uwe unatafuta matangazo ya redio za mtandaoni kutoka Japini aku kupata picha kutoka Macedonia, Global Voices ni kijiji cha mtandaoni kinachowaleta watu kila siku kupashana habari, picha, maoni kutoka kwenye pembe zao za dunia na kukuunganisha. Ni matumaini yetu kwamba utashiriki kwenye mazungumzo haya. www.globalvoicesonline.org

Blogging Postively: Jihusishe

Kuna njia nyingi za kushiriki katika jumuiya ya Blogging Postively. Kama ungependa kujumuishwa katika ramani yetu ya wanablogu wanaoishi na VVU duniani kote tafadhali tuma barua pepe kwa Juhie Bhatia Mhariri wa Afya ya Umma wa Global Voices [http://globalvoicesonline.org/author/juhie-bhatia/] huku ukituma kiungo cha blogu yako na mji unamoishi. Pia unahimizwa kujiunga na orodha ya kupokea barua [http://groups.google.com/group/rv-positively]

Shukurani

Shukurani kwa wote ambao walishiriki katika kutayarisha mwongozo huu, ikiwa ni pamoja na kupitia vipindi vya mazungumzo ambavyo viliunda msingi wa mradi wa "Blogging Positively". Shukurani maalumu ziende kwa: David Sasaki, Solana Larsen, na Juhie Bhatia wa Rising Voices na Global Voices, Daudi Were (Kenyan Blogs Webring, KenyaUnlimited, na Mental Acrobatics), na Serina Kalande, ambao ni wanablogu wa Kenya ambao kwa pamoja walipendekeza kuanzishwa kwa mradi; Dennis Kimambo na Collins Oduor wa REPACTED (Kenya); Andrius Kulikauskas wa Maabara Minciu Sodas kwa Independent thinkers (Lithuania); Maureen Agena wa WOUGNET (Uganda); Sylvie Niombo wa AZUR Development (Jamhuri ya Kongo), Finch Brian (Acid reflux , Canada), Louise Binder (Jumuiya Kimataifa ya Wanawake wanaoishi na VVU/UKIMWI, Canadian Treatment Action Council, Canada); Jamie Uhrig wa HIM (USA na Myanmar), Dhojo Wahengbam wa HIVNetwork (India), na Tobias Eigen wa Kabissa (Afrika). Washiriki kwenye mazungumzo walikuwa ni pamoja na: Glenna Gordon, Amira Hussaini, Deborah Dilley, Eduardo Avila, Salam Adil, Jeremy Clarke, Jillian York, Mialy Andriamananjara, Ljubisa Bojic, Jogany, Maria Joyce, Fred Kayiwa, Luihamu Ringo, Taline Haytayan, Himakshi Piplani, Eric Bleich, Nekesa Were, Lova Rakotomalala, Anas, Patrick Karanja, Victor Ngeny, Rezwan, Sylwia Presley, Senfuka Samweli, Tom Ochuka, Wendi Losha Bernadette, Teekay Ndiba, James Leahy, Sasha Mrkailo, Leah Okeyo, Zoneziwoh Mbondgulo, Konaté Boukary, Leung, Stephen McGill, Kiyavilo Msekwa, Veronica Kalambi. Daudi Were (Mental Acrobatics, http://www.mentalacrobatics.com/think/) ambaye alibuni jina la mradi, "Blogging Positively," ambalo kwako tunamshukuru sana. Maabara ya Andrius Kulikauskas na Minciu Sodas zilifanya ukarimu wa kutoa bure nafasi ya mtandaoni ya kufanya mazungumzo yetu, ambayo yalizalisha mambo mengi tuliyoyatumia kuandaa Mwongozo huu. Solana Larsen na Juhie Bhatia wamefanya kazi kubwa katika kutayarisha ramani ya "Blogging Positively", na Juhie aliandika baadhi "Visa vya Utafiti" vya mwanzo kama nyenzo kwa ajili ya tovuti ya Rising Voices. David Sasaki amekuwa chanzo cha kudumu cha msaada, miitikio yenye manufaa, na kutoa moyo "wa kiuchungaji". Serina Kalande amekuwa ni "Mtunzaji motomoto" akitusaidia kuendeleza harakati hii toka mwanzo hadi mwisho.

- Janet Feldman, Mhariri na Mtayarishaji wa Mwongozo wa Blogging Positively | www.kaippg.org na www.actalive.org

Mwongozo huu umetafsiriwa na Collins Oudour na kisha kuhakikiwa na Deogratias Simba.

Kublogu kwa ajili ya kuleta Sera bora zaidi nchini Ukraine

Pavel Kutsev, ambaye ni kiongozi katika harakati za kupunguza madhara nchini Ukraine na mwanzilishi mwenza wa shirika lisilo la kifaida la Drop-in Center, hutumia blogu yake kupambana na unyanyapaa na kujenga welewa kuhusu mahitaji ya kiafya ya waliyo nayo raia wa Ukraine wanaoishi na hali ya kuathiriwa na dawa za kulevya na VVU/UKIMWI. Pavel anatetea haki za watumiaji wa dawa za kulevya ambao wanashiriki katika program za tiba mbadala, ambazo zinalenga kuwashawishi watumia dawa wasitumie kwa kujidunga sindano, ili kupunguza kasi ya kuenea kwa janga la VVU/IKIMWI. Kutsev, ambaye anaishi na VVU, anaelewa vizuri kuhusu unyanyapaa na ubaguzi ambao unawakabili watumia dawa za kulevya na wenye VVU. Katika Blogu yake, Pavel hushughulikia masuala mbalimbali ambayo hujadiliwa na jamii ya Waukraine ya watumiaji wa dawa za kulevya za kudunga, ikiwemo aina ya dawa za kimatibabu, huduma za afya na msaada, na harakati za kisiasa kupinga maamuzi ya hivi karibuni katika baadhi ya manispaa za Ukraine ya kupiga marufuku baadhi ya tiba mbadala. Aidha, Kutsev huchapisha simulizi zinazohusu wasifu wake kwa ajili ya kushirikisha mafunzo aliyopata na wasomaji wake. Kutsev anasema kuwa blogu imemsaidia yeye na shirika lake kusikika na kuwa na ushawishi mkubwa zaidi. Amealikwa kushiriki kama mtaalamu wa kikosi kazi chenye jukumu la kuunda sera ya tiba mbadala, na anaamini kuwa Wizara ya Afya ya Ukraine ilianzisha sera yake ya sasa ya kufanya baadhi ya tiba mbadala za dawa za kulevya kupatikana katika maduka ya dawa kama mwitiko kwa majadiliano katika ulimwengu wa blogu wa Waukraine. Kutsev anafanya kazi kuhakikisha kwamba rasilimali ya mtandao ya kimataifa ya kuunganisha juhudi za wanaharakati wa kupunguza madhara na kuendeleza tiba mbadala, kama njia ya kupunguza maambukizi ya VVU / UKIMWI.

http://depo3p.livejournal.com/

http://rising.globalvoicesonline.org/grantees/dropin-center/

Knight Foundation

OPEN SOCIETY INSTITUTE

RisingVoices

Rising Voices ni vuguvugu la uandishi wa habari wa kiraia wazo lililoanzishwa na Global Voices na uendeshaji wake unategemea msaada wa hisani ya Taasisi ya John S. na James L. Knight na vilevile Taasisi ya Open Society. Unaruhusiwa kunakili, kusambaza na kutumia kazi hii na hata kuitumia kubuni kazi nyingine ili mradi ukumbuke kukiri mchango wa Rising Voices.